# CHANGAMOTO ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA KISWAHILI KAMA LUGHA YA PILI KATIKA SHULE ZA UPILI NCHINI RWANDA: MFANO WA SHULE TEULE WILAYANI MUSANZE

**Faustin Ndikubwimana**

Rwanda Polytechnic

ndikubwimanafaustin@gmail.com

## Ikisiri

*Makala hii inalenga kujadili changamoto zinazowakumba walimu na wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili nchini Rwanda, mfano wa shule teule za upili wilayani Musanze. Aidha, makala hii iliongozwa na Nadharia ya Viwezeshi katika ufundishaji wa lugha iliyoasisiwa na Gibson katika mwaka wa 1977. Vilevile, wakati wa ukusanyaji wa data, mtafiti alitumia ushuhudiaji, usaili na uchanganuzi matini kama mbinu za kukusanya data. Walengwa walikuwa walimu na wanafunzi kutoka shule teule za G S Muhoza I na Ecole de Sciences de Musanze, wilayani Musanze. Data za watafitiwa zilifanyiwa uchanganuzi na matokeo yalibainisha kuwa walimu na wanafunzi wote hukumbwa na changamoto tofauti wakati wa ufundishaji wa Kiswahili. Changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa nyenzo za kufundishia na kujifunzia, ujuzi finyu wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi, ukosefu wa mafunzo kwa walimu na mtazamo hasi wa wanafunzi kuhusu lugha ya Kiswahili. Makala, inapendekeza kuboresha ufundishaji wa Kiswahili nchini kwa kuchapisha vitabu vingi zaidi, kutoa mafunzo kwa walimu wa Kiswahili na kuongeza idadi ya vipindi vya Kiswahili. Pia, kuhakikisha kuwa Kiswahili kinatahiniwa katika mitihani ya taifa kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha tatu.*

**Dhana za Msingi**: Ujifunzaji, Ufundishaji, Lugha ya Pili, Shule za Upili

## 1.0 Utangulizi

Mabadiliko katika mbinu za ufundishaji hujitokeza na kufanywa ili kuakisi mahitaji ya wanafunzi na teknolojia. Kiswahili ni lugha mojawapo kati ya lugha ambazo hutumiwa na watu tofauti wa mataifa mbalimbali hapa duniani. Baadhi ya mataifa duniani yenye mwamko wa kufundisha na kujifunza lugha ya Kiswahili ni Uingereza, Ujerumani, Japani, Marekani na nchi za Afrika ya Mashariki na Kati (Saleh, 2019).

Kiswahili kinatumika kama lugha ya pili nchini Rwanda na ni muhimu katika ajira, biashara, elimu, na diplomasia (Crystal, 1997; Niyomugabo, 2016). Historia ya ufundishaji wa Kiswahili nchini Rwanda imepitia mabadiliko, ikianzia utawala wa Wajerumani mnamo mwaka 1907 na kuachwa na Ubelgiji baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia (Mlaga, 2017; Ntawiyanga, 2020). Baada ya uhuru, serikali ya Rwanda ilifanya juhudi za kukuza Kiswahili, hasa kwa kushirikiana na Tanzania (Mlaga, 2017). Hata hivyo, licha ya juhudi hizo, Kiswahili kilikosa nafasi kubwa katika mtaala hadi baada ya mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi.

Baada ya mauaji ya kimbari ya Watutsi, Kiswahili kilijumuishwa katika mtaala wa shule. Tangu mwaka 2008, serikali imeendelea kuimarisha Kiswahili, kikifundishwa kama somo la lazima kuanzia kidato cha kwanza hadi cha tatu, na katika ngazi za juu kwenye michepuo ya lugha, jambo linaloonyesha dhamira ya serikali ya kukuza lugha hii (Mlaga, 2017). Hii ni ishara ya kwamba Kiswahili kinachukuliwa kama chombo cha kuleta umoja na kuimarisha mahusiano ya kimataifa, hasa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, na hivyo kuleta faida kubwa katika jamii ya Rwanda. Isitoshe, REB (2015) inabainisha kuwa Kiswahili kimejumuishwa katika mtaala wa shule za sekondari nchini Rwanda na kinafundishwa kutoka kidato cha kwanza hadi cha tatu. Hata hivyo, somo hili haliorodheshwi kati ya masomo ya kutahiniwa kitaifa katika ngazi hii. Kiswahili huanza kutahiniwa rasmi kutoka kidato cha nne hadi cha sita, hasa katika michepuo ya lugha.

Licha ya juhudi zinazofanywa na serikali ya Rwanda katika kuimarisha elimu, bado kuna changamoto mbalimbali zinazokumba ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili, kama ilivyo katika nchi nyingine za Afrika. Tafiti zilizopita zinaonyesha kuwa uhaba wa vifaa vya kufundishia unaathiri kwa kiasi kikubwa mafanikio ya wanafunzi na walimu. Kwa mfano, Mutheu (2019)

anaeleza kuwa vifaa vya kujifunzia vina mchango mkubwa katika kufanikisha ufundishaji bora, huku Farrant (2006) akisisitiza kuwa vifaa duni vinaweza kuathiri vibaya utendaji wa wanafunzi. Kwa mtazamo huu, ingawa vifaa ni muhimu, juhudi zaidi zinapaswa kuelekezwa si tu katika upatikanaji wake bali pia katika matumizi bora ya nyenzo hizo kwa ajili ya ufundishaji unaomlenga mwanafunzi.

Badugela (2012) anabaini kuwa shule nyingi za Afrika Kusini zinakabiliwa na upungufu wa nyenzo za kufundishia Kiingereza kama lugha ya pili, hali inayoashiria kuwa Kiswahili kinaweza kukumbwa na matatizo yanayofanana. Vilevile, Harumi (2011) anabainisha kuwa walimu hukumbana na vikwazo vikubwa katika ufunzaji wa lugha ya pili kutokana na ukosefu wa nyenzo bora, jambo linaloathiri moja kwa moja maendeleo ya wanafunzi. Hili linadhihirisha kuwa changamoto za lugha ya pili si za Kiswahili pekee, bali ni suala la jumla linalohitaji sera madhubuti za elimu na uwekezaji wa rasilimali. Kwa muktadha huu, ushirikiano kati ya serikali, wadau wa elimu, na walimu binafsi unaweza kusaidia kupunguza matatizo haya.

Aidha, tafiti mbalimbali zimeonyesha kuwa mitazamo ya wanafunzi na jamii pia inaathiri ujifunzaji wa Kiswahili. Utafiti wa Miima na Kawoya (2021) nchini Uganda unaonyesha kuwa wananchi wengi wanapendelea Kiingereza na lugha za kienyeji badala ya Kiswahili, hali inayosababisha changamoto katika utekelezaji wa sera za lugha. Kwa upande mwingine, Mohochi na wenzake (2019) wanaeleza kuwa wanafunzi wakimbizi katika kambi ya Dadaab, Kenya, wana mitazamo hasi kuhusu Kiswahili, jambo linalokwamisha ufanisi wa ufundishaji wa lugha hiyo. Kwa mtazamo huu, hili linaonyesha kuwa utekelezaji wa Kiswahili kama lugha ya pili unapaswa kuambatana na mabadiliko ya kijamii na utamaduni. Bila jamii kuona thamani ya Kiswahili, jitihada za serikali na taasisi za elimu zitakuwa na mafanikio madogo.

Nchini Rwanda, Niyomugabo (2016) anabainisha changamoto zinazokumba ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili, kama vile uchache wa walimu, ukosefu wa nyenzo, na matatizo ya kimazungumzo na kimaandishi. Ingawa utafiti wake umechangia kuelewa changamoto hizi, haukubainisha mikakati ya kukabiliana nazo wala kujadili mazingira ya kufundisha Kiswahili kwenye shule kama G.S. Muhoza na Ecole de Sciences de Musanze. Serikali ya Rwanda kupitia

REB imechukua hatua kama vile uandikaji wa vitabu na kufundisha Kiswahili kutoka kidato cha kwanza hadi cha tatu, lakini bado kuna changamoto zinazokwamisha mafanikio ya ufundishaji.

Licha ya juhudi za serikali ya Rwanda katika kukuza Kiswahili, ufundishaji na ujifunzaji wake katika shule za sekondari bado unakabiliwa na changamoto kama uhaba wa walimu, ukosefu wa vifaa vya kufundishia, na mtazamo hasi wa jamii. Aidha, kutokutahiniwa kwa Kiswahili katika mitihani ya kitaifa kwa kidato cha kwanza hadi cha tatu huathiri motisha ya wanafunzi, huku upungufu wa rasilimali ukiendelea kudhoofisha mafanikio ya lugha hii katika mtaala.

Kwa kuzingatia hali hii, utafiti uliozalisha makala hii ulilenga kuchunguza changamoto zinazowakumba walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule teule za sekondari wilayani Musanze, Rwanda. Lengo likiwa ni kubainisha hali halisi ya ufundishaji wa Kiswahili, na kupendekeza mikakati ya kuboresha mazingira ya kujifunza lugha hii.

## 2.0 Muhtasari wa Mapitio ya Maandiko

Kwa jumla maandiko mengi yanaonesha kuwa kuna changamoto kuu tatu katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya pili nchini Rwanda. Mosi, kuna uhaba wa nyenzo za kufundishia kujifunzia. Pili, kuna changamoto za kisera na tatu kuna mtazamo usiofaa kwa baadhi ya walimu na wanafunzi. Tafiti zinaonesha kuwa vitabu vya Kiswahili ni vichache, vifaa vya kisasa havipo, na serikali haijatoa rasilimali za kutosha kuboresha mazingira ya ujifunzaji. Pia, walimu wengi hawana mafunzo ya kutumia teknolojia inayoweza kusaidia wanafunzi kujifunza Kiswahili kwa njia shirikishi na ya kuvutia.

Kwa upande wa sera ya lugha, Kiswahili hakijapewa kipaumbele katika mitihani ya taifa wala katika matumizi ya kiserikali, jambo linalopunguza ari ya kujifunza lugha hii. Mtazamo hasi wa baadhi ya wanafunzi na walimu kuhusu umuhimu wa Kiswahili unachangia kupungua kwa motisha ya kujifunza.

### 2.3 Changamoto Zinazohusiana na Mtazamo wa Wanafunzi na Walimu Kuhusu Kiswahili

Mtazamo hasi kuhusu Kiswahili ni changamoto kubwa inayozuia ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha hii. Katika muktadha wa Rwanda, Kiswahili kinachukuliwa kama somo la

pili linalopewa kipaumbele kidogo, jambo linalosababisha wanafunzi kutokuthamini umuhimu wake. Kulingana na Gichure (2020), mtazamo hasi kuhusu Kiswahili unadhoofisha motisha ya wanafunzi na ufanisi wa kujifunza. Wanafunzi wanapohisi kuwa Kiswahili hakina umuhimu katika mitihani ya taifa na katika maisha yao ya kila siku, wanapoteza hamu ya kujifunza na kutumia Kiswahili kwa ufanisi. Haitema (2002) anasema kuwa mtazamo hasi unadhihirisha kikwazo kikubwa katika mchakato wa kujifunza lugha, kwani wanafunzi hutumia juhudi kidogo kujifunza lugha wanayoiona kuwa haileti manufaa ya moja kwa moja.

Aidha, ni muhimu kuzingatia kuwa mtazamo chanya unaweza kuwa na athari kubwa kwa mafanikio ya wanafunzi katika kujifunza Kiswahili. Walimu wana jukumu muhimu la kubadilisha mtazamo wa wanafunzi kwa kutumia mbinu za ufundishaji zinazowapa motisha na zinazowavutia. Mbinu hizi ni pamoja na kuelezea umuhimu wa Kiswahili katika maisha ya kila siku, katika biashara, na kama sehemu muhimu ya utamaduni wa Afrika Mashariki. Pia, kuonesha faida za Kiswahili katika soko la ajira, ambapo katika maeneo mengi ya Afrika Mashariki, Kiswahili kinahitajika kama lugha ya mawasiliano katika sekta mbalimbali, kutakuwa na manufaa makubwa kwa wanafunzi. Kwa kuongeza, Kiswahili kinatoa fursa nyingi za kiutamaduni na kijamii kwa wanafunzi wanaojua lugha hii vizuri.

Kwa hivyo, walimu wa Kiswahili wanapaswa kutumia mbinu za ufundishaji zinazojenga mtazamo chanya kuhusu lugha hii, ikiwa ni pamoja na kutumia mifano ya maisha halisi ya wanafunzi, kuhusisha Kiswahili na masuala ya kijamii na kiuchumi, na kuwaonyesha wanafunzi jinsi Kiswahili kinavyoweza kuwa na manufaa kwa maisha yao ya baadaye. Hii itaongeza hamu ya kujifunza Kiswahili na itaongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha hii nchini Rwanda.

## 3.0 Methodolojia na Nadharia ya Utafiti

Methodolojia ya utafiti ni njia mbalimbali zinazotumiwa na mtafiti kwa kutatua tatizo la utafiti (Kothari, 2004). Vilevile, mkabala wa utafiti uliozalisha makala hii ulikuwa wa kitaamuli ambapo mtafiti aliziweka na kuzipanga taarifa kutokana na maudhui au makundi yanayofanana. Mtafiti alikuwa bayana na makini kwa kufafanua, kueleza, kuvumbua, kufanya majaribio,

kuhakiki data alizopata kupitia usanifu wa utafiti. Data zilizopatikana kwa walengwa zilichambuliwa kwa kina kwa njia za kimaelezo.

Aidha, mtafiti alitumia mbinu ya ushuhudiaji ili kukusanya data za msingi zinazohusiana na lengo la kubainisha changamoto zinazowakabili walimu na wanafunzi wakati wa ufunzaji na kufunza Kiswahili kama lugha ya pili. Aina ya ushuhudiaji uliotumiwa ni ushuhudiaji shirikishi ambao ulimlazimu mtafiti kwenda uwandani kushuhudia mambo yote yanayotendeka katika madarasa ya kidato cha pili A na kidato cha tatu A na B huku washuhudiwa wakiwa hawatambui lengo la mtafiti kwenye G.S Muhoza I na Ecole de Sciences de Musanze wilayani Musanze. Madarasa haya yaliteuliwa kwa njia lengwa kwa kuwa ndiyo madarasa tu yanayopatikana kwenye shule hizo. Mtafiti alishuhudia jinsi ufundishaji wa Kiswahili unavyotendeka katika madarasa teule. Kupitia njia hii, mtafiti alichunguza jinsi Kiswahili kinavyofundishwa na kujifunza darasani. Hii ilijumuisha kurekodi masomo, kuangalia vitabu vya kiada, na kufuatilia mwenendo wa ufundishaji.

Isitoshe, mtafiti alifanya mahojiano kwa njia lengwa na watafitiwa ambao ni walimu watatu wanaofundisha Kiswahili. Walimu hawa waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa kwa kuwa ndio wanaofundisha Kiswahili kwenye shule hizo. Aidha, walichaguliwa kupitia usampulishaji lengwa ili kupata ufahamu wa kina kuhusu changamoto zinazowakabili katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Pia, mtafiti aliwapata kupitia usampulishaji sinasibu wanafunzi watatu wa darasa la tatu A na watatu wa darasa la tatu B wa G.S Muhoza I na wanafunzi watatu wa kidato cha pili A kutoka E.SC. Musanze kwa kurikodi taarifa zinazohusu changamoto zinazokumba ufunzaji na kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili katika shule hizo wilayani Musanze, nchini Rwanda. Wanafunzi hawa walioteuliwa katika usaili walichaguliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa kulingana na kiwango cha ufaulu wa Kiswahili darasani. Pamoja na hayo, kulikuwa na wale ambao wanaweza kujitetea vizuri na wale wanaojieleza kidogo.

Nadharia iliyoongoza utafiti uliozalisha makala hii ni Nadharia ya Viwezeshi. Nadharia hii iliasisiwa na Gibson katika mwaka wa 1977. Hii ni nadharia ya ufunzaji wa lugha ya pili inayodai kuwa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha hujengwa na viwezeshi. Gibson

(1977) anafafunua kuwa viwezeshi ni kama vitu vinavyoonesha uwezekano wa vitendo ambavyo mtumiaji huweza kuvitumia katika kazi yake. Katika hali hii, viwezeshi vinaweza kuhusishwa na vitu kama vile majengo ya shule yaani miundombinu za shule, maktaba, mitaala, kamusi na upatikanaji wa vitabu vya kutumia na wanafunzi na walimu, kompyuta, televisheni, redio pamoja na maabara ya lugha.

Mihimili ya Nadharia ya Viwezeshi katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili inajumuisha uzingatiaji wa mtumiaji, muktadha, na lugha. Uzingatiaji wa mtumiaji unahusisha umuhimu wa walimu wenye ujuzi wa Kiswahili ili kusaidia wanafunzi kujifunza kwa ufanisi. Uzingatiaji wa muktadha unahimiza matumizi ya mazingira sahihi na vifaa vya kufundishia vinavyowezesha ujifunzaji bora wa lugha. Uzingatiaji wa lugha unahusiana na matumizi sahihi ya Kiswahili bila kuchanganya na lugha nyingine, isipokuwa pale inapohitajika kusaidia uelewa. Nadharia hii inaangazia changamoto kama ukosefu wa vifaa, athari za lugha ya kwanza, na uwezo wa walimu, hivyo kusaidia kuboresha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

Nadharia ya Viwezeshi ilifaa katika utafiti uliozalisha makala hii kwani inatoa mfumo wa kuelewa na kushughulikia changamoto zinazozuia ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Inasisitiza umuhimu wa mazingira ya kufundishia, vifaa, na rasilimali kama vitabu na teknolojia. Katika muktadha wa Rwanda, changamoto kama ukosefu wa vifaa, walimu wenye ujuzi, na athari za lugha nyingine huathiri ujifunzaji wa Kiswahili. Nadharia hii husaidia kuchunguza changamoto hizi na kutoa mapendekezo ya kuboresha mazingira ya ufundishaji ili kuimarisha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili.

## 4.0 Matokeo ya Utafiti

Ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili katika shule za upili nchini Rwanda unakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri ufanisi wa mchakato wa elimu. Walimu na wanafunzi wanakumbana na vikwazo mbalimbali vinavyoathiri upataji na ustadi wa lugha hii. Pamoja na juhudi za serikali ya Rwanda katika kuimarisha matumizi ya Kiswahili, bado kuna changamoto zinazotokana na uhaba wa wanafunzi wenye ujuzi wa kutosha, ukosefu wa mafunzo kwa walimu wa Kiswahili, upungufu wa vifaa vya kujifunzia, na muktadha wa lugha unaoathiri motisha na ushiriki wa wanafunzi.

### 4.1 Changamoto za Walimu na Wanafunzi katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili

Utafiti uliozalisha makala hii umebaini changamoto zinazowazuia walimu na wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji wa somo la Kiswahili. Changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji, ujuzi finyu wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi, ukosefu wa mafunzo kwa walimu, idadi ya vipindi vichache pamoja na ukosefu wa utashi wa kujifunza Kiswahili kwa wanafunzi.

#### 4.1.1 Uhaba wa Vifaa vya Kufundishia

Uhaba wa vifaa vya kufundishia huwasukuma walimu kutumia mbinu za kufundishia ambazo hazilengi wanafunzi. Data za ushuhudiaji zimebainisha kuwa walimu na wanafunzi wanakabiliwa na changamoto ya uhaba wa nyenzo za ufundishaji kama vile vitabu vya Kiswahili na kamusi. Idadi ya vitabu vya Kiswahili vya kidato cha tatu vilikuwa vichache kulingana na idadi ya wanafunzi. Kwa mujibu wa Muteu (2019), upungufu wa nyenzo za kufundishia hufanya ufundishaji wa lugha kuwa mgumu. Hii maana yake ni kwamba ukosefu wa nyenzo ni hasara kwa wanafunzi na hata kwa walimu wao. Aidha, wahojiwa walibainisha kuwa uhaba wa nyenzo unaathiri sana ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

Uhaba wa vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji ni changamoto inayokabili na kuathiri malengo ya ufundishaji. Ambuko & Odera (2013) wanasema kuwa upungufu wa nyenzo huathiri ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Hii inamaanisha kuwa walimu wasipotumia nyenzo za ufundishaji vitaathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Vilevile, walimu na wanafunzi wanakumbwa na changamoto ya kamusi kwa kuwa katika ushuhudiaji, tuliona kuwa hawatumii ipasavyo kamusi wakati wa ufundishaji wa somo la Kiswahili kama lugha ya pili. Kwa hiyo, hali hii ya kutokuwa na vifaa vya kufundishia na kujifunzia inaathiri sana ushiriki wa wanafunzi katika somo la Kiswahili.

Data za usaili pia zilibainisha kuwa kuna uchache wa nyenzo za kufundisha Kiswahili kama lugha ya pili miongoni mwa walimu na wanafunzi. Mbito (2013) anabainisha kwamba upungufu wa vitabu vya kiada ni changamoto inayowakabili walimu na wanafunzi katika mchakato wa

kufundisha Kiswahili katika shule za sekondari. Kwa hali hii, rasilimali duni huwafanya walimu kutumia mbinu za kufundishia ambazo hazilengi wanafunzi. Changamoto ya kutokuwa na vifaa vinavyotosha inaelezwa na mwalimu Umulisa wa shule ya kwanza kwa kusema kuwa:

Mimi kama mwalimu ninakabiliwa na vikwazo vya uhaba wa vitabu vya kufunzia na kutokuwa na kamusi ambazo zinaweza kutusaidia katika hali ya kusomesha na kujifunza kwa upande wa walimu na wanafunzi. Hapa shuleni kuna vitabu vichache sana kulingana na idadi ya wanafunzi (Mwalimu Umulisa, utafiti 2023).

Maelezo haya ya mwalimu Umulisa yanaonesha kuwa kufunza na kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili kunakabiliwa na uhaba wa vifaa na uhaba huo unaathiri vibaya hali ya ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa upande wa walimu na kwa upande wa wanafunzi. Kwa mujibu wa Nadharia ya Viwezeshi ili Mwalimu awe na ufanisi wa kazi yake inashauriwa awape wanafunzi vitabu vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi ili waweze kumudu somo hata wakiwa wao wenyewe (Akaka, 2017). Hali hii inatupa mwangaza wa kuwa kufundisha Kiswahili kama lugha ya pili kunahitaji kupatikana kwa vifaa vinavyotosha ili malengo ya ufundishaji yafikiwe. Kwa hiyo, uhaba wa vifaa vya ufundishaji unaweza kusababisha upungufu wa ubora wa elimu kwa wanafunzi.

#### 4.1.2 Ujuzi Finyu wa Lugha ya Kiswahili kwa Wanafunzi

Kupitia mbinu ya ushuhudiaji, tulibaini kuwa baadhi ya wanafunzi huwa na changamoto ya kueleza mawazo yao katika lugha ya Kiswahili pamoja na kuchanganya lugha ya Kiingereza au Kinyarwanda. Wanafunzi huathiriwa na lugha ya Kinyarwanda na Kiingereza. Isitoshe, data za usaili zinabainisha kuwa wanafunzi wanakumbwa na tatizo la ujuzi finyu wa lugha. Ujuzi mdogo wa kuzungumza lugha ya Kiswahili huathiri wanafunzi wanapokuwa darasani kama inavyobainishwa na mwanafunzi wa shule katika madondoo yafuatayo:

Sisi wanafunzi tunakabiliwa na changamoto ya kukosa ujuzi wa kutosha wa mazungumzo ya Kiswahili. Licha ya kuwa somo rasmi katika mtaala, bado kuna ugumu mkubwa wa kutumia lugha hii kwa ufasaha katika mazungumzo ya kila siku (Hakimana, utafiti 2023).

Wanafunzi wenzangu mara nyingi huogopa kuongea Kiswahili kwa sababu wanahisi kuwa hawana msamiati wa kutosha, wanahofia makosa ya kisarufi, au hawana mazoezi ya kutosha ya kuzungumza lugha hii katika mazingira yao ya kila siku (Aline, utafiti 2023).

Dondoo hili linabainisha kuwa wanafunzi wa shule zilizofanyiwa utafiti hawana misingi ya mazungumzo kuhusu somo la Kiswahili kama lugha ya pili. Wanafunzi waliohojiwa walichanganya lugha zikiwemo Kiswahili, Kiingereza na Kinyarwanda. Kiwango cha wanafunzi watafitiwa katika mazungumzo kingali chini. Aidha, data za mahojiano zinabainisha kuwa wanafunzi hawamudu vizuri stadi ya kuzungumza Kiswahili na wanaogopa wanapoongea Kiswahili kwa kuwa si lugha yao ya kwanza.

Vilevile, katika ushuhudiaji, tulibaini kuwa hakuna sera ya lugha kwenye shule ambazo utafiti ulifanyika. Miima na Kawoya (2021) wanaeleza kuwa kutokuwa na sera ya lugha inayofuatilia matumizi ya ufundishaji na mawasiliano ya Kiswahili shuleni ni changamoto inayojitokeza katika baadhi ya shule nyingi. Kwa hali hii, viongozi wakiweka sera ya lugha kwenye shule zao, wanafunzi hawatakabiliwa na changamoto ya kuzungumza Kiswahili kwa kuwa wanatumia muda mwingi katika kuzungumza lugha ya Kiingereza.

Saleh (2019) anasema kuwa wanafunzi wanakabiliwa na changamoto ya kuzungumza lugha ya kwanza katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili wakati ambapo somo linaendelea. Hali hii ni changamoto inayoweza kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa sababu matumizi ya lugha ya kwanza mara nyingi hupunguza nafasi ya mazoezi ya Kiswahili na kuwafanya wanafunzi kutegemea tafsiri badala ya kufikiria moja kwa moja kwa Kiswahili. Vilevile, wanafunzi wanapozungumza Kinyarwanda wakati wa somo la Kiswahili, wanakosa fursa za kutumia Kiswahili kwa vitendo. Hii inafanya lugha ya Kiswahili kubaki ya kinadharia badala ya kuwa nyenzo ya mawasiliano halisi.

### 4.1.3 Ukosefu wa Mafunzo kwa Walimu wa Lugha ya Kiswahili

Data za mahojiano na walimu zinadhihirisha kuwa mafunzo au semina ni muhimu lakini walimu wa Kiswahili hawapewi mafunzo hayo kama walimu wa masomo mengine ya Sayansi na

Kiingereza. Dondoo hili linaelezwa na mwalimu wa Kiswahili kutoka shule ya kwanza kwa kusema kuwa:

Tangu nilipoingia kazini katika mwaka 2010 sijapata hata mafunzo kuhusu somo la Kiswahili. Hatupati mafunzo kama walimu wengine wa Sayansi na Kiingereza. Kwa hiyo, hali ya kutopewa mafunzo kama walimu wengine ni changamoto kubwa na inaathiri ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili (Mwalimu Muhire, utafiti 2023).

Dondoo hili linabainisha kuwa walimu wa Kiswahili hawapati mafunzo kuhusu somo hili la Kiswahili. Maoni ya mwalimu huyu yanaungwa mkono na Akaka (2017) kwa kusema kuwa walimu wanapata shida nyingi kwa sababu hawapati mafunzo kuhusu ufundishaji wa Kiswahili. Aidha, maoni ya Akaka (khj) yanathibitishwa na Mlaga (2017) kwa kusema kwamba ukosefu wa mafunzo ya mara kwa mara ili kuboresha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji katika lugha ya Kiswahili unakwamisha utumiaji, uwezekano na maarifa mapya yanayoonekana katika stadi za Kiswahili.

Hali ya kukosekana kwa mafunzo kwa walimu wa Kiswahili kama walimu wa Sayansi na Hisabati inaathiri ufundishaji wa Kiswahili. Hali ya kutoandaliwa mafunzo kwa walimu wa Kiswahili inaathiri ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama inavyosisitizwa na walimu watoa taarifa. Hali hii ya kutopata semina inaathiri ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili hususani kuhusu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, Nadharia ya Viwezeshi inasisitiza umuhimu wa walimu kupata mafunzo ya mara kwa mara na kuwa mwalimu asiyekuwa na mafunzo endelezi hatekelezi vema ufundishaji wake kuwa elimu haina mwisho. Walimu wakipata mafunzo kuhusu ufundishaji wa Kiswahili wataboresha ufundishaji wa lugha ya Kiswahili.

### 4.1.4 Idadi ya Vipindi Vichache vya Somo la Kiswahili

Katika ushuhudiaji, tulibaini kwenye ratiba za walimu kuwa Kiswahili kina saa mbili kwa wiki. Kimsingi, saa hizi hazitoshi kulingana na mada zinazopatikana katika silabasi. Isitoshe, mahojiano na watoa taarifa ambao ni walimu wa Kiswahili wote walisema kuwa wanakumbwa na changamoto ya saa zilizotengwa kwa somo la Kiswahili. Saa za somo la Kiswahili ni chache

kulingana na yaliyomo katika silabasi ya Kiswahili kama wanavyobainisha walimu wa somo kwa kusema:

Sisi walimu wa Kiswahili tunakumbwa na changamoto kubwa ya kutomaliza silabasi kwa wakati kutokana na muda mfupi uliotengwa kwa somo hili katika ratiba za masomo. Kwa kawaida, Kiswahili kimepewa saa chache kwa wiki, mara nyingi zikiwa ni saa mbili pekee, muda ambao hautoshi kufundisha na kujadili kwa kina mada zote zilizopangwa katika silabasi (Mwalimu Muhire, utafiti 2023).

Kutopewa muda wa kutosha katika ratiba ni kikwazo kikubwa kwetu. Hali hii inasababisha ugumu katika utoaji wa maelezo ya kina, uendelezaji wa mijadala shirikishi darasani, na ufuatiliaji wa maendeleo ya wanafunzi (Umulisa, utafiti 2023).

Maelezo haya ya msailiwa mwalimu yanaonesha kuwa ujumuishaji wa mtaala wa Kiswahili kwa muda uliopangwa unaleta kazi kubwa kwa walimu na kwa wanafunzi. Hii ina maana kwamba walimu na wanafunzi hukimbilia juu ya silabasi, hivyo ufundishaji na ujifunzaji haufanyiki ipasavyo. Watoa taarifa kama watu wanaopatikana uwandani walibainisha mapengo yanayopatikana katika silabasi hiyo zikiwemo kuwa muda uliotengwa kwa ufundishaji wa Kiswahili. Walimu walieleza kuwa saa za kufundishia Kiswahili ni chache kulingana na yaliyomo katika silabasi. Hali hii huwafanya walimu kutomaliza kufundisha mada zote kwa kuwa muda wa kufundisha mada hizo hauendani na yaliyomo au mada zinazofunzwa.

Taarifa za walimu zinabainisha kuwa silabasi ni pana kwa kiasi kikubwa kulingana na yaliyomo na saa zinazofunzwa Kiswahili kwa wiki. Akaka (2017) anaeleza kuwa Kiswahili hukabiliwa na changamoto ya kuwa na saa chache kwa wiki. Vilevile, changamoto hii imeungwa mkono na Mushumbwa (2022) anaposema kuwa mada za Kiswahili zinapangwa bila ya kuangalia uwiano wa mada hizo na saa zilozotengewa somo la Kiswahili. Muda uliotengewa kufundishia Kiswahili hautoshi kulingana na masomo mengine kama vile Kiingereza.

Akaka (khj) anaendelea kusema kuwa somo la Kiswahili lina vipengele vyote vya sarufi, fasihi na uchambuzi wake kama vile vinavyopatikana katika somo la Kiswahili. Hali hii inabainika kuhusu somo la Kiswahili kwa kuwa nchini Rwanda, Kiswahili hufundishwa vipindi viwili kwa

wiki wakati ambapo Kiingereza hufunzwa vipindi sita kwa wiki (REB, 2015). Hali hii ya idadi ya vipindi vichache vya somo la Kiswahili ni changamoto inayokwamisha ujifunzaji mzuri wa lugha hii kama lugha ya pili katika shule za upili nchini Rwanda. Aidha, wakati masomo mengine kama Kiingereza yanaweza kuwa na vipindi vingi, Kiswahili mara nyingi hupata nafasi ndogo katika ratiba ya shule. Jambo hili linaathiri umahiri wa wanafunzi katika kuzungumza, kusoma, na kuandika lugha hii kwa ufasaha.

### 4.1.5 Ukosefu wa Utashi na Mtazamo Hasi wa Kujifunza Kiswahili kwa Wanafunzi

Katika ushuhudiaji, ilibainika kuwa walimu wanakumbwa na shida ya kufundisha wanafunzi wa kidato cha tatu, hususani katika muhula wa tatu, kwa sababu somo la Kiswahili halitatahiniwa katika mitihani ya taifa. Hali hii husababisha changamoto katika utoaji wa masomo kwani wanafunzi wengi hupunguza bidii katika kujifunza, wakizingatia zaidi masomo ambayo wanajua kuwa yatakuwa sehemu ya mtihani wa mwisho wa kitaifa. Vilevile, usaili uliofanywa kwa walimu wa Kiswahili katika shule ulibainisha kuwa walimu hukumbwa na changamoto ya kuwahamasisha wanafunzi kusoma kwa bidii, kwani mara nyingi wao huona somo hilo kama halina umuhimu wa moja kwa moja katika matokeo yao ya mwisho. Kutokana na mtazamo huu, baadhi ya walimu hujikuta wakipambana na hali ya kutopewa kipaumbele kwa somo la Kiswahili, jambo ambalo linaweza kuathiri ubora wa ufundishaji na uelewa wa wanafunzi katika lugha hii muhimu. Hii ni kusema kuwa hakuna uwezashaji wa kutosha wa kisera na kisiasa. Vilevile, hali hii inaashiria haja ya mkazo zaidi katika kufundisha Kiswahili kwa kuhakikisha kuwa linasisitizwa kama somo muhimu, hata kama halihusishwi katika mitihani ya taifa. Haya yalielezwa na walimu kwa kusema:

Walimu tunakumbwa na shida ya kwamba wanafunzi wa kidato cha tatu hawana utashi wowote wa kujifunza Kiswahili hususani katika muhula wa tatu wa kumaliza mwaka. Ni changamoto kubwa kwa sisi walimu kwa kuwa wanafunzi wanafahamu somo halitatahiniwa katika mitihani ya taifa (Mwalimu, Kamana, utafiti 2023).

Aidha, watafitiwa wengi aliunga mkono hoja hii kwa kusema kwa kunaomba *National Examination and School Inspection Authority* (NESA) ipange namna ya kutayarisha somo la Kiswahili kama masomo mengine. Mahojiano na wanafunzi wa shule ya pili ya bweni

yalibainisha kuwa wanafunzi hawana utashi wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili kwa kuwa lugha hii ya Kiswahili haitahiniwi katika mtihani ya taifa. Aidha, Niyomugabo (2016) anaeleza kuwa viongozi hawana utashi wa kulishughulikia somo la Kiswahili kwa kuwa halitahiniwi katika mitihani ya taifa. Maelezo ya Niyomugabo (khj) yanaendana na mahojiano baina ya wanafunzi na mtafiti kwa kuwa wanafunzi walimweleza mtafiti kuwa wao wanakosa utashi wa kujifunza Kiswahili kwa kuwa somo hili halitahiniwi katika mitihani ya taifa.

Isitoshe, baadhi ya wanafunzi waliohojiwa walishindwa kujieleza kwa Kiswahili ndipo wakaanza kuchanganya lugha. Akaka (2017) anasema kuwa mtazamo walio nao wanafunzi kuhusu somo la Kiswahili ni changamoto ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa kuwa wao hupendeleza masomo yanayokuwa na hadhi ya juu kama vile udaktari, uhandisi, sayansi na kuchukua Kiswahili kama lugha ya kawaida na kupuuza Kiswahili na kukizingatia kama kozi zinazopatikana kuwa za hali ya chini. Tatizo hili la wanafunzi kutotilia mkazo kujifunza lugha ya Kiswahili linachangiwa na sera ya serikali ya kutotahini Kiswahili katika mitihani ya taifa.

Vilevile, Ndikubwimana (2023) anasema kuwa wanafunzi wanapinga somo la Kiswahili kwa kuwa halitahiniwi katika mitihani ya taifa kwa ngazi ya chini ya shule za upili. Aidha, Mbito (2013) anasema kuwa mtazamo hasi wa wanafunzi kuhusu somo fulani huathiri ufaulu. Kulingana na maoni ya wataalamu hao, wanafunzi hupuuza somo la Kiswahili kwa kuwa halitahiniwi katika mitihani ya taifa, na hali hii huathiri ujifunzaji wa somo hili ipasavyo.

**5.0 Hitimisho na Mapendekezo**

Utatifi uliozalisha makala hii ulikuwa ni wa kitaamli unaotumia maneno kwa kueleza na kufafanua matokeo ya utafiti. Vilevile, mtafiti alitumia ushuhudiaji, usaili na uchanganuzi matini kama mbinu za kukusanya data. Data zilizochambuliwa kupitia ushuhudiaji, mahojiano na upitiaji wa matini mbalimbali zilibainisha kuwa walimu na wanafunzi hukabiliwa na changamoto nyingi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili zikiwemo uhaba wa vifaa vya ufunzaji na ujifunzaji.

Utafiti pia umebaini kuwa walimu hawapewi mafunzo ya mara kwa mara ili kuboresha mbinu za ufundishaji wao. Vilevile, wanafunzi wanapuuza lugha ya Kiswahili kwa kuwa wana mtazamo

hasi wa kuwa somo la Kiswahili halitahiniwi katika mitihani ya taifa wanapomaliza kiwango cha tatu. Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa walimu na wanafunzi wanakuwa na changamoto ya kuwa somo la Kiswahili halitahiniwi katika mitihani ya taifa. Hali ambayo inasababisha somo hili kupuuzwa kwa kuwa tayari wanafunzi wanaelewa kuwa halitatahiniwa. Pia, utafiti huu uligundua kuwa walimu wanakabiliwa na changamoto ya idadi ya vipindi vichache vya somo la Kiswahili na muda finyu wa somo la Kiswahili ambao huathiri sana mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili na ni mzigo kwa walimu na wanafunzi.

Kutokana na mjadala wa utafiti uliozalisha makala hii, tunapendekeza hatua mbalimbali ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili nchini Rwanda. Kwanza, serikali kupitia wizara ya elimu inapaswa kuhakikisha upatikanaji wa vitabu, vifaa vya kufundishia, kamusi mbalimbali, pamoja na msaada wa kidijitali. Hatua hii itasaidia walimu na wanafunzi kupata nyenzo sahihi za kujifunzia na hivyo kuboresha umahiri wao katika Kiswahili. Pili, kuna umuhimu wa kuimarisha mafunzo ya walimu wa Kiswahili kwa kuwaandaa na mbinu bora za kufundisha wasio wazungumzaji wa asili. Mafunzo haya yanapaswa kuzingatia mikakati ya kufundisha Kiswahili kwa wanafunzi wa viwango tofauti na jinsi ya kushughulikia changamoto zinazojitokeza katika ujifunzaji. Tatu, ni muhimu kuongeza muda wa ufundishaji wa Kiswahili shuleni. Hii ni kwa sababu muda mfupi wa kufundisha Kiswahili huathiri uelewa wa wanafunzi. Kwa hiyo, ni muhimu kwa Bodi ya Elimu nchini Rwanda kupanga saa za kutosha ili somo la Kiswahili lipate nafasi sawa na masomo mengine kama Kiingereza na Sayansi.

Nne, Kiswahili kinapaswa kuwa somo la lazima na kitahiniwe katika mitihani ya taifa. Ikiwa Kiswahili kitaingizwa katika mitihani ya taifa, wanafunzi wataongeza juhudi za kujifunza, hali ambayo itaongeza idadi ya wazungumzaji wa Kiswahili nchini Rwanda. Tano, serikali inapaswa kujenga maabara za lugha ya Kiswahili. Maabara hizi zitawasaidia walimu na wanafunzi kuboresha mawasiliano na umahiri wao katika matumizi ya Kiswahili. Mazingira ya kujifunzia yanapoboreshwa, wanafunzi wanakuwa na nafasi kubwa ya kuelewa lugha kwa ufasaha. Mwisho, tunapendekeza matumizi rasmi ya Kiswahili katika sekta zote za serikali kama ilivyo kwa Kinyarwanda, Kiingereza, na Kifaransa. Kwa sasa, lugha hizi zinatumika katika matangazo ya serikali, ofisi za umma, na nyaraka mbalimbali, lakini Kiswahili hakijapewa nafasi sawa.

Hivyo, serikali inapaswa kuhakikisha Kiswahili kinatumika rasmi ili kukuza nafasi yake katika mawasiliano ya kitaifa na kikanda.

Marejeleo

Akaka, L. (2017). *Changamoto zinazowakabili walimu katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya*. Kioo cha Lugha, Juz. 11, Na. 1, uk. 47–57.

Ambuko, B., & Odera, F. (2013). Selection and media in teaching-learning of Kiswahili language in secondary schools in Kenya. *International Journal of Information and Communication Technology Research*, *3*(1), 12–18.

Badugela, T.M. (2012). Problems Facing Educators in Implementing the National Curriculum Statement: The Case Study of Tshifhena Secondary School. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri (haijachapishwa). Pretoria: University of South Africa.

Bodi ya Elimu ya Rwanda. (2015). *Muhtasari wa Somo la Kiswahili*: Kidato ch 4-6, Michepuo ya Lugha, Kigali.

Crystal, D. (1997). *English as a Global Language.* Cambridge: Cambridge University Press.

Farrant, J.S. (2006). *Principles and Practice of Education*. United Kingdom: Longman Group Limited.

Gibson, J.J. (1977). *The Theory of Affordances in Gibson, Perceiving, Acting and Knowing, Hillsdale.* Lawrence Erlbaum.

Gichure, C.N. (2020). *Factors Contributing to Poor Performance in Kiswahili subject among Secondary Schools Students in Marmanet Location in Laikipia County in Kenya* (Bachelor's Dissertation). Kenya. Gretsa University.

Haitema, T.B. (2002). *Student Attitudes Vis a Vis Foreign Language in Elementary Schools (EFLS): A Longitudinal Study*. Chapel Hall: University of North Carolina.

Harumi, S. (2011). Classroom silence: Voices from Japanese English as foreign language learners. *ELT Journal*, *65*(3), 260–269.Kothari, C. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques* (2nd Edition). New Delhi: New Age International Limited Publishers.

Mbito, J. (2013). Challenges Facing Teachers and Students in the Process of Teaching and Learning Kiswahili in Public Secondary in Kiambu District in Kiambu County. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Miima, F. A., & Kawoya, V. F. (2021). Mstakabala na changamoto za Kiswahili nchini Uganda. *East African Journal of Swahili Studies*, *3*(1), 70–77.

Mlaga, W. K. (2017). Historia ya Kiswahili nchini Rwanda: Kielelezo cha utashi wa kisiasa. *Kioo cha Lugha*, *15*, 1–19.

Mohochi, S. M., Mukuthuria, M., & Ontieri, J. O. (2019). Kiswahili katika elimu ya juu. Sura ya tisa: Ufundishaji wa Kiswahili kwa wakimbizi katika kambi ya Kakuma na Dadaab: Changamoto na mwelekeo mpya. *Moi University Press*, 121–128.

Mushumbwa, A. R. (2022). Changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari za umma Tanzania: Mfano wa shule teule za sekondari wilaya ya Kwimba. *Jarida la CHALUFAKITA*, *4*, 31–50. https://dx.doi.org/10.4314/jclfkt.v4i1.3

Mutheu, W. A. (2019). *An assessment of challenges and strategies in teaching and learning of Kiswahili in public secondary schools in Hamisi Sub-County* (Tasnifu ya Shahada ya Umahiri isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Maseno.

Muthii, S. (2002). Language policy and education: A regional conference held in Nairobi from 15th–17th May 2006.

Ndikubwimana, F. (2023). *Changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili nchini Rwanda: Mfano wa shule teule wilayani Musanze* (Tasnifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Rwanda.

Niyomugabo, C. (2016). Ufundishaji wa Kiswahili katika shule za Rwanda: Historia, tathmini ya makosa, matatizo na mahitaji. *Kiswahili*, *79*(1), 78–92.

Ntawiyanga, S. (2020). Makosa ya upatanishi wa kisarufi katika ujifunzaji wa lugha ya pili: Mfano wa wanafunzi wa shule za upili wilayani Muhanga, nchini Rwanda. *Kioo cha Lugha*, *17*, 15–32.

Oladejo, J. A. (1993). Error Correction in ESL: Learner's Preferences. *TESOL Canada Journal*, 10(2), 71-89. https://doi.org/10.18806/tesl.v10i2.619

Saleh, H. F. (2019). *Changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni katika darasa mseto la wingilugha* (Tasnifu ya Shahada ya Umahiri isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Shani, S. K. (2019). *Changamoto zinazowakabili walimu katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni katika stadi ya kusoma* (Tasnifu ya Shahada ya Umahiri isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.